JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO**

# TAARIFA KWA UMMA

**ORODHA YA MAZAO YA MIKUNDE NA MBEGU ZA MAFUTA YATAKAYOUZWA KWA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI NA MINADA YA KIDIJITALI KWA MWAKA 2025.**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) inapenda kuwataarifu wakulima, wafanyabiashara, na wadau wote kwa ujumla katika sekta ya mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko kuwa mazao yafuatayo jamii ya mikunde na mbegu za mafuta yatauzwa kupitia mfumo wa stakabadhi za ghala kwa njia ya minada ya kidijitali (TMX) katika **mikoa yote ya Tanzania Bara katika msimu wa 2024/2025**. Mfumo huu unalenga kuhakikisha uwazi, usalama na ufanisi katika biashara ya mazao.

**Mazao yanayohusika yameorodheshwa:**

| Na. | Zao | Mwanzo wa msimu wa mauzo |
|---|---|---|
| 1 | Choroko | Januari 2025 |
| 2 | Ufuta | Aprili 2025 |
| 3 | Dengu | Juni 2025 |
| 4 | Mbaazi | Juni 2025 |
| 5 | Soya | Mei 2025 |

Mwanzo rasmi wa msimu wa mauzo kwa kila zao katika mazao haya utatangazwa na COPRA hivyo wakulima, wafanyabiashara na wadau wote wa mazao hayo watatakiwa kufuata miongozo ya mazao ya jamii ya mikunde na mfumo wa mauzo uliowekwa kwa ajili ya kuuza na kununua mazao jamii ya mikunde kama ilivyoainishwa kwenye kiunganishi https://www.copra.go.tz/publications/guidelines na kuhakikisha wanauza na kununua mazao katika msimu utakaotangazwa na Mamlaka.

Kwa maelezo ya ziada tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe: info@copra.go.tz.

Imetolewa na:

Irene M. Mlola

**MKURUGENZI MKUU**

*Jengo la Kahawa Plaza, Mtaa wa Njedengwa, S.L.P 2780, Dodoma -Tanzania.*
*Simu: +255 26 2310225, Barua pepe: info@copra.go.tz.*